



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**TAARIFA KWA UMMA**

**KUHUSU UTEUZI WA MADIWANI WANAWAKE WA VITI MAALUM**


**Dodoma, 01 Novemba, 2022**

Katika kikao chake cha tarehe 29 Oktoba, 2022, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuzingatia kifungu cha 86A(1) ya Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, kikisomwa pamoja na kifungu cha 35 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287 na kifunga cha 19 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura ya 288, imewateua Madiwani wanawake wa Viti Maalum kumi (10) kujaza nafasi wazi za Madiwani katika Halmashauri kumi (10) za Tanzania Bara.

Uteuzi huo umefanyika baada ya Tume kupokea barua kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, yenye Kumb. Na. CCB.126/443/01 ya tarehe 12 Septemba, 2022, akiitarifu Tume kuhusu uwepo wa nafasi wazi za Madiwani Wanawake wa Viti Maalum katika Halmashauri 10 za Tanzania Bara zilizotokana na vifo.

**Madiwani Wanawake wa Viti Maalum walioteuliwa ni kama ifuatavyo:-**

| NA. | JINA                        | CHAMA | HALMASHAURI                          |
|-----|-----------------------------|-------|--------------------------------------|
| 1.  | Ndugu Lidia Loves Msongole  | CCM   | Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya       |
| 2.  | Ndugu Mariam Robert Makasi  | CCM   | Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa     |
| 3.  | Ndugu Bahati Hussein Shaban | CCM   | Halmashauri ya Wilaya ya Nzega       |
| 4.  | Ndugu Sauda Juma Irumba     | CCM   | Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua      |
| 5.  | Ndugu Theresia Lucas Mlay   | CCM   | Halmashauri ya Wilaya ya Moshi       |
| 6.  | Ndugu Monica John Madiwa    | CCM   | Halmashauri ya Wilaya ya Handeni     |
| 7.  | Ndugu Hadija Mussa Ngope    | CCM   | Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba  |
| 8.  | Ndugu Hapines Msengi Kingu  | CCM   | Halmashauri ya Wilaya ya Iramba      |
| 9.  | Ndugu Zainabu Abdi Mabrouck | CCM   | Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa      |
| 10. | Ndugu Zainabu Bakari Orty   | CCM   | Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam |

  
 Dkt. Wilson M. Charles  
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**  
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**